**Mkataba wa Vienna Unaohusu Hifadhi ya Tabaka la Ozoni na Itifaki ya Montreal kuhusu udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

## 1. Utangulizi

Mkataba wa Vienna unaohusu hifadhi ya Tabaka la Ozoni ulisainiwa na nchi wanachama mwaka 1985. Mkataba huu ulilenga kuweka ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama katika kupeana taarifa za tafiti kuhusu maendeleo ya tabaka la Ozoni lililokuwa limeanza kumo'ngonyoka. Mkataba wa Vienna haukuwa na mamlaka ya kisheria ya kudhibiti uharibifu wa tabaka hususan udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la ozoni. Ili kuweka mamlaka ya kisheria, mnamo mwaka 1987 nchi wanachama wa Mkataba wa Vienna zilitia saini Mkataba mdogo (Itifaki) ya Montreal inayohusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni, ambapo Tanzania iliridhia mwaka 1993.

## 2. Lengo la Mkataba na Itifaki

Lengo la Mkataba wa Vienna ni kulinda Tabaka la Ozoni na kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yanayotokana na kuharibiwa kwa tabaka la Ozoni.

Lengo la Itifaki ya Montreal ni kudhibiti kemikali zinazomongónyoa tabaka la Ozoni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yanayotokana na kuharibiwa kwa tabaka la Ozoni.

## 3. Ushiriki wa mikutano

(i) Mkutano wa maandalizi ya Mkutano Mkuu wa nchi wanachama wa Itifaki ya Montreal ambao hufanyika kila mwaka.

(ii) Mkutano Mkuu wa nchi wanachama wa Itifaki ya Montreal hufanyika kila mwaka.

(iii) Mkutano Mkuu wa Nchi wanachama wa Mkataba wa Vienna ambao hufanyika kila baada ya miaka miwili.

(iv) Vikao vya Kamati Tendaji ya Mfuko wa utekelezaji wa Itifaki ya Montreal ambavyo hufanyia mara mbili kwa mwaka.

## 4. Majukumu ya nchi wanachama

(i) Uandaaji na uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba na Itifaki.

(ii) Uchangiaji wa hiyari kwenye Mfuko wa utekelezaji wa Itifaki ya Montreal.

**5. Faifa za mkataba**

(i) Kulinda afya ya binadamu kwa kupungua kwa mionzi mikali ya ultraviolet inayofikia uso wa dunia, ambayo husababisha magonjwa kama saratani ya ngozi, mtoto wa jicho na kudhoofika kwa kinga mwilini.

(ii) Kulinda Mazingira kwa kupunguza madhara kwa viumbe hai kama samaki, planktoni, na mazao ya kilimo kutokana na tabaka la ozoni lililoimarika ambalo hupunguza mionzi ya ultraviolet katika uso wa dunia.

(iii) Kuchangia katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi

(iv) kupunguza uzalishaji wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni ambazo pia ni gesijoto zenye uwezo mkubwa wa kuchangia ongezeko la joto duniani, kama vile Hydrofluorocarbons (HFCs).

(v) Kuchangia juhudi za kimataifa za kupunguza gesi joto, hivyo Kusaidia kufikia malengo ya Mkataba wa Paris.

(vi) Kuwezesha upatikanaji wa teknolojia mbadala kwa kupokea teknolojia na vifaa rafiki kwa tabaka la ozoni kupitia ufadhili wa Mfuko wa Itifaki ya Montreal (Multilateral Fund), ambayo inasaidia kuboresha sekta za viwanda, kilimo, viyoyozi na majokofu.

(vii) Kupunguza utegemezi wa teknolojia zenye athari kubwa kwa mazingira.

(viii) Kukuza Ushirikiano wa Kimataifa na nchi zingine kupitia programu za mafunzo, kubadilishana uzoefu, na miradi ya pamoja ya mazingira inayotekelezwa chini ya mwavuli wa Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal.

(ix) Tanzania imeimarisha mfumo wa sera, sheria, na taratibu zinazolenga hifadhi ya mazingira, ikiwa ni pamoja na kudhibiti uagizaji na matumizi ya kemikali zinazoharibu tabaka la ozoni.

(x) Kuongeza uelewa wa jamii juu ya umuhimu wa kulinda tabaka la ozoni kupitia kampeni za uhamasishaji.

(xi) Kuboresha Sekta ya Majokofu na Viyoyozi kwa utekelezaji wa miradi ya kuboresha teknolojia ya majokofu na viyoyozi kwa kutumia viyoyozi na majokofu yasiyoharibu tabaka la ozoni.

(xii) Kuimarika kwa ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini kwa kutumia teknolojia rafiki kwa mazingira."

**6. Shughuli/miradi inayotekelezwa chini ya mkataba**

(i) Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Marekebisho ya Kigali unaolenga kupunguza matumzi ya kemikali jamii ya HFCs.

(ii) Utekelezaji wa shughuli wezeshi ya kujenga uwezo wa kitaasisi katika kutekeleza Itifaki ya Montreal kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni.

(iii) Utekelezaji wa Mpango wa kuondosha kemikali jamii ya Hydrochlorofluorocarbons (HCFCs), 2023- 2030;

(iv) Maadhimisho ya Siku ya Kiataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni ambayo hufanyika tarehe 16 Septemba kila mwaka.

(v) Shughuli wezeshi ya ukusanyaji wa taarifa za kemikali chakavu zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal nchini na maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Usimamizi wake.

(vi) Mafunzo kwa maafisa wa Idara za Serikali na mawakala wa forodha katika mipaka mbalimbali ya nchi pamoja na viwanja vya ndege kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa kemikali na vifaa vinavyodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal.

(vii) Mafunzo kwa mafundi mchundo wa viyoyozi na majokofu kuhusu namna bora ya kuhudumia vifaa hivyo pasipo huathiri mazingira.

(viii)

## 7. Mafanikio ya utekelezaji wa mkataba

(i) Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi kutoka mifuko ya kimataifa na wadau wa maendeleo

(ii) Kuimarisha ushirikiano na jumuiya ya kimataifa katika nyanja za utafiti na uendelezaji wa teknolojia za hifadhi ya tabaka la ozoni na mabadiliko ya tabianchi.

(iii) Kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na fedha za miradi zinazoletwa nchini

(iv) Kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu hifadhi ya tabaka la ozoni, mabadiliko ya tabianchi na athari zake Upatikanaji wa fursa za mafunzo kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali pamoja na wakufunzi kuhusu hifadhi ya tabaka la ozoni na mbadiliko ya tabianchi

## 8. Changamoto zinazokabili utekelezaji wa mkataba

- Gharama kubwa za teknolojia na vifaa vya kutambua kemikali/gesi zinazoharibu tabaka la ozoni na kuchangia ongezeko la joto duniani.

- Uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi tabaka la ozoni.

- Uhaba wa vifaa vya kutambua kemikali/gesi zinazoharibu tabaka la ozoni pamoja na mitambo ya kusafisha gesi.